

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2015 CERTIFIED



**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MAMLAKA YA
MAWASILIANO TANZANIA KUANZIA JULAI 2021 HADI SEPTEMBA 2022**

1.0 UTANGULIZI

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ni Taasisi ya Serikali yenyewe jukumu la kusimamia Sekta ya Mawasiliano nchini Tanzania. Sekta ya Mawasiliano inajumuisha Utangazaji, Simu na Intaneti, na Posta. TCRA ilianzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Namba 12 ya mwaka 2003 baada ya kuunganishwa kwa iliyokuwa Tume ya Utangazaji Tanzania (TBC) na Tume ya Mawasiliano Tanzania (TCC). TCRA ilianza kutekeleza majukumu yake tarehe 1 Novemba 2003.

1.1 Kazi na Majukumu ya TCRA kwa Mujibu wa Sheria

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 5 cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na. 12 ya 2003, TCRA ina wajibu wa: -

- (i.) Kuhimiza ushindani bora na uchumi wenye tija;
- (ii.) Kulinda haki na maslahi ya watumiaji;
- (iii.) Kuhamasisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa watumiaji wote ukijumuisha watumiaji wenye kipato kidogo, walioko vijiji na watumiaji ambao wako katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara;
- (iv.) Kuimarisha elimu kwa umma, uelewa na kuzifahamu huduma zinazosimamiwa na TCRA; na
- (v.) Kuhakikisha umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira.


Aidha, kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na *Sheria ya Mawasiliano Kielektroniki na Posta Na. 3 ya Mwaka 2010*, majukumu ya TCRA ni pamoja na: -

- a) Kutoa leseni, kuongeza muda wa leseni na kufuta leseni pale ambapo masharti ya leseni husika hayaafuatwi;
- b) kuweka viwango kwa bidhaa na huduma zinazosimamiwa;
- c) kuweka viwango, kanuni na masharti ya kusambaza bidhaa na huduma zinazosimamiwa;
- d) kudhibiti viwango na bei ya jumla ya mawasiliano kati ya mitandao.
- e) Kufuatilia utendaji na mwenendo wa Sekta ya Mawasiliano;
- f) Kuwezesha kutatuliwa kwa malalamiko na migogoro baina ya Watoa huduma na kati ya Mto huduma na Mtumiaji wa huduma;
- g) Kusambaza taarifa kuhusu mambo ambayo ni muhimu kwa ajili ya shughuli za TCRA;
- h) Kufanya mashauriano na taasisi nyingine za udhibiti, Bodi au Taasisi zenye majukumu yanayofanana na yale ya TCRA katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nje ya nchi;
- i) Kutoa leseni na kusimamia mifumo ya mawasiliano ya kielektroniki na Posta.

TCRA ina Ofisi Tanzania Bara na Visiwani kama inavyoonekana hapa chini:-

KANDA	MIKOA
OFISI YA ZANZIBAR	Unguja (Kaskazini na Kusini), Pemba (Kaskazini, Kusini), Unguja Mjini Magharibi
MASHARIKI	Dar es Salaam, Morogoro, Lindi, Pwani na Mtwara
KASKAZINI	Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga
ZIWA	Mwanza, Geita, Kagera, Shinyanga, Mara, Simiyu
KATI	Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma
NYANDA ZA JUU KUSINI	Mbeya, Songwe, Iringa, Ruvuma, Rukwa, Katavi, Njombe

Shughuli za Mamlaka ya Mawasiliano zinagusa wadau wakuu watatu ambao ni **Serikali** yenyeye jukumu la kutoa sera na sheria; **watoa huduma** wanaopewa leseni na masharti ya leseni na **TCRA**, na watumiaji wa huduma za mawasiliano ambao TCRA ina jukumu la kulinda maslahi yao.



Taasisi ambazo ni wadau wa moja kwa moja na TCRA kiutendaji ni pamoja na Tume ya Utangazaji Zanzibar (ZBC), Vyombo ya kusimamia sheria (Polisi, Mahakama), Tume ya Ushindani wa Biashara (FCC), Baraza la Ushindani (FCT), Baraza la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC), Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Msaliji wa Hazina, n.k.

1.2 Dira, Dhamira na Lengo Kuu la Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

1.2.1 Dira: Kuwa na jamii iliyowezeshwa na huduma zenyeye hadhi ya kimataifa za mawasiliano ya kielektroniki na posta.

1.2.2 Dhamira: Kusimamia huduma za mawasiliano ya kielektroniki na posta kwa kukuza ushindani, ufanisi wa uchumi, na upatikanaji wa huduma bora kwa wote pamoja na kulinda maslahi ya wadau kwa ustawi ya jamii ya Tanzania.

1.2.3 Lengo Kuu: Kuimarisha mawasiliano kwa wote na upatikanaji wa huduma nafuu za kielektroniki na posta.

1.3 Sekta ya Mawasiliano na Mchango wake Kiuchumi

Sekta ya Mawasiliano ni Sekta wezeshi inayochangia kukua na kuendelea kwa sekta nyingine. Huduma na bidhaa za Mawasiliano ni za msingi katika maisha ya wananchi kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Kutokana na mchango huo, Sekta ya Mawasiliano imekuwa ya kimkakati na ya msingi katika maendeleo ya uchumi wa kidijiti na uchumi wa buluu nchini Tanzania; kuanzia ngazi ya mtu binafsi, ngazi ya Kaya, Taasisi na Kitaifa.

Utoaji wa huduma za mawasiliano ni wa ushindani hivyo umesababisha kuongezeka kwa idadi ya mitandano, TEHAMA na aina za huduma zinazotolewa kwa Wananchi, Taasisi na Serikali kwa ujumla. Kuenea kwa huduma hizi kunawezeshwa na uwepo wa Sera imara, sheria nzuri na mifumo wezeshi ya kiusimamizi na utoaji leseni.

TCRA imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (FYDP III) kwenye sekta ya mawasiliano, ambayo utekelezaji wake unahusisha mchango wa TCRA kwenye uchumi kama ifuatavyo: -

- a) Kuimarisha miundombinu ya mawasiliano na upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa lengo la kuboresha kiuchumi wa kidijiti na uchumi wa buluu;
- b) Kuendelea kuweka mazingira bora ya ushindani kwenye sekta ya mawasiliano ili wananchi wengi waweze kumudu ghamama za huduma za mawasiliano;
- c) Kulinda watumiaji wa huduma za mawasiliano dhidi ya uhalifu mtandaoni kwa kutumia mifumo ya kiusimamizi; na
- d) Kugawa masafa na kutoa leseni kwa watoa huduma zinazowezesha kuongeza idadi ya watumiaji wa intaneti ili kufikia lengo la asilimia 80 ifikapo 2025.

2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

2.1 Utoaji wa Leseni

TCRA imeendelea kutoa Leseni na kusimamia masharti ya leseni kwa watoa huduma za mawasiliano nchini. Tangu kuanzishwa kwake hadi kufikia Septemba 2022, TCRA imetoka leseni zifuatazo:

Jedwali Na 1: Leseni zilizotolewa

Na.	AINA YA LESENI	IDADI YA LESENI
1	Miundombinu ya Mawasiliano (Network Facility License)	22
2	Utumiaji wa Miundombinu ya Mtando (Network Services)	10
3	Matumizi ya Huduma (Application Services)	107
	Huduma za Maudhui (Content Services)	741
	✓ Televisheni	61
4	✓ Televisheni za Mtandaoni (Online TV)	390
	✓ Cable TV	65
	✓ Redio	218
	✓ Redio za Mtandaoni (Online radio)	7
5	Posta na Ushafirishaji Vifurushi (Postal & Courier Services)	91
	✓ Mto Huduma wa Umma (Shirika la Posta Tanzania)	1
	✓ Kampuni binafsi za usafirishaji (Couriers)	90
6	Leseni ndogo za Ufungaji na Utengenezaji; Uingizaji na Usambazaji wa Vifaa vyta Simu; VSAT; Masafa ya VHF/HF	2,161
JUMLA		3,132

2.2 Usimamizi wa Shughuli za Mawasiliano ya Simu na Intaneti

TCRA inasimamia shughuli za Mawasiliano ya Simu na Intaneti kwa kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano ya simu na intaneti zinatolewa kwa kuzingatia viwango vyta kitaifa na kimataifa na viwango vilivyowekwa kwenye sheria ya EPOCA na kanuni zilizopo. Kupitia Kanuni zilizopo TCRA inahakikisha kuwa huduma za mawasiliano ya simu na Intaneti zinakidhi ubora wa huduma unaotakiwa kitaifa na kimataifa pamoja na kuhakikisha kuwa udanganyifu kwenye huduma za simu na intaneti unadhibitiwa. Aidha, TCRA inahakikisha kuwa watumiaji wa huduma za mawasiliano na intaneti wanasajiliwa na hivyo kuboresha utoaji wa huduma zinazotolewa kwao. TCRA imeendelea na usimamizi wa Mawasiliano ya Simu na Intaneti kwa kutumia mifumo usimamizi kama ifuatavyo:-

Mifumo ya Usimamizi wa Mawasiliano ya simu na Intaneti

Ili kuwezesha usimamizi kwenye mawasiliano ya simu, Serikali kupitia TCRA ilianzisha mfumo uitwao Tele-Traffic Management System (TTMS). Mfumo wa TTMS ni mfumo wa

kusimamia na kuratibu mawasiliano ya simu wenye uwezo wa kubaini takwimu mbalimbali zinazopita katika mitandao ya mawasiliano. Mfumo wa TTMS unachukua taarifa kutoka kwenye mifumo ya watoa huduma, unazichakata na kutoa taarifa zinazowezesha TCRA kusimamia majukumu yake ya kiudhibiti pamoja na uhakiki wa mapato ya watoa huduma za mawasiliano. Aidha, umechangia kuongeza ufanisi katika uratibu wa utekelezaji wa sheria na kanuni zinazosimamia sekta ya mawasiliano nchini. Moduli ambatishi ndani ya mfumo wa TTMS zinawezesha yafuatayo: -

- a. **Usimamizi wa simu za ndani na za kimataifa:** Moduli hii inaiwezesha TCRA kupata takwimu za mawasiliano yanayofanyika ndani na nje ya nchi (international and local traffic). Kwa kutumia mfumo huu, TCRA inapata takwimu za mawasiliano ya simu za ndani yaliyofanyika baina ya wateja wa mitandao tofauti (kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine – “off-net calls”) na ndani ya mtandao mmoja (“on-net calls”), pamoja na simu za kimataifa zinazoingia na kutoka nchini.
- b. **Kubaini simu za ulaghai (Anti-fraud Management System):** Moduli hii inawezesha kubaini simu za kilaghai za ndani ya nchi na zinazotoka nje ya nchi kwa kutumia utaratibu kwa simu za majaribio pamoja na uchakataji wa taarifa nyingi “Big Data Analysis”. Hivyo kurahisisha ufuatiliaji na udhibiti wa udanganyifu kwenye mitandao ya simu.
- c. **Kanzidata ya Namba Tambulishi (Central Equipment Identity Register):** Moduli hii inawezesha uhakiki wa vifaa vyote vinavyounganishwa na mitandao ya watoa huduma kama vinakidhi viwango vya kimataifa na ni salama kwa watumiaji. Moduli hii imeweza kuzuia matumizi ya simu zilizoripotiwa kuibiwa, kupotea au kuharibika pamoja na kuzuia matumizi ya simu zisizokuwa na viwango. Usimamizi huu unawezesha kubaini na kufungia namba tambulishi za vifaa vya Mawasiliano zilizonakiliwa (Duplicate IMEIs), namba tambulishi za vifaa vilivyotumika kwenye udanganyifu pamoja na namba tambulishi zilizotolewa taarifa ya kupotea au kuibiwa. Kwa mfano, Kuanzia Julai 2021 hadi kufikia Septemba 2022 jumla ya namba tambulishi zilizofungiwa na mfumo huu ni 52,087 ambazo ziliripotiwa kupotea, kuibiwa au kuhusika katika matukio ya kihalifu, hivyo kuwezesha kupunguza matukio ya wizi na kusaidia upatikanaji wa vifaa vya Mawasiliano vyenye ubora kwenye soko.

- d. **Usimamizi wa Miamala ya Fedha (Mobile Money Monitoring):** Moduli hii inawezesha kusimamia taarifa za huduma za miamala ya fedha kupitia mitandao ya simu. Pia inasaidia kuhakiki ukusanyaji wa mapato ya serikali kupitia kodi, tozo zinazotokana na miamala ya fedha inayofanyika kupitia mitandao ya simu. Vilevile kuwezesha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za miamala hivyo kurahisisha usimamizi wa sekta ya fedha.
- e. **Ufuatiliaji wa Miamala ya Watoa Huduma za Malipo (Aggregators Monitoring):** Moduli hii inawezesha kufuatilia mwenendo wa idadi na thamani ya miamala inayopitishwa na watoa huduma za malipo kama vile Selcom, Cellulant na Azam Pay. Taarifa hii inaiwezesha TCRA kufuatilia mwenendo wa ukuaji wa huduma za malipo kupitia mitandao ya simu. Vilevile kuwezesha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za miamala hivyo kurahisisha usimamizi wa sekta ya fedha.
- f. **Kuhakiki Mapato yatokanayo na Huduma za Mawasiliano ya Simu:** Moduli hii inawezesha kuhakiki mapato yatokanayo na huduma za mawasiliano ambazo ni kupiga simu, kutuma jumbe fupi na matumizi ya intaneti, pamoja na huduma nyingine zinazotumia mitandao ya simu.
- g. **Kanzidata ya taarifa za Usajili wa Laini za Simu:** Kanzidata ya usajili wa laini za simu inatunza taarifa za usajili wa laini za simu kutoka kwa watoa huduma. Kanzidata hii imeunganishwa na kanzidata za watoa huduma zinazotunza taarifa za usajili wa laini za simu. Pia, kanzidata hii imeunganishwa na Kanzidata ya Mamlaka ya Vitambulisho Vya Taifa (NIDA) ili kuhakiki tarifa zinaletwa kama ziko sahihi.
- h. **Ufuatiliaji wa ubora wa huduma za mawasiliano (Quality of Service):** Ufuatiliaji wa ubora wa huduma unafanyika kwa kutumia vifaa vya ukaguzi vilivyofungwa kwenye magari maalumu. Pia, TCRA imeanza kuboresha mfumo unaowezesha ufuatiliaji wa ubora wa huduma za mawasiliano kwa nchi nzima kwa kuchakata taarifa zinazopatikana moja kwa moja kutoka kwenye miundombinu ya watoa huduma.

- i. **Ufuatiliaji wa taarifa za miundombinu ya watoa huduma:** Moduli hii inaweza kufuatilia miundombinu ya mawasiliano kama vile usambaaji wa minara, miundombinu ya mkongo (fiber optic) pamoja na vituo vya kuhifadhi taarifa (Data centers) hivyo kupelekea kutambua ufikiwaji wa huduma katika maeneo mbalimbali nchini. Taarifa hii inaiweza TCRA kutambua minara inayofanya kazi, maeneo ilipo na teknolojia inayotumia.

2.3 Usimamizi wa Shughuli za Utangazaji

Utangazaji ni njia pekee ya Mawasiliano inayowafikia watu wengi kwa haraka na wakati mmoja. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Wizara yenyeye dhamana ya sekta ndogo ya Utangazaji ina wajibu wa kuweka mazingira rafiki ya kusambaza huduma za Utangazaji kwa njia ya redio, televisheni na mitandao nchi nzima ili kumfikia kila mwananchi. Hali kadhalika Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina wajibu wa kuhakikisha kuwa maudhui yanayorushwa na vituo vya Utangazaji yanazingatia maadili na weledi wa uandishi wa habari na pia hayakiuki Sheria na Kanuni zinazosimamia sekta ya Utangazaji. Ni wajibu wa Mamlaka kuhimiza utengenezaji, uzalishaji na usambazaji wa maudhui ya ndani (local content) na kutangaza urithi, vivutio, mila na **desturi za mtanzania**.

2.4 Usimamzi wa Shughuli za Posta

Shughuli za posta zinahusisha usafirishaji na usambazaji wa barua, nyaraka, vipeto na vifurushi kutoka kwa watumaji kupitia makampuni ya posta. Usimamizi wa shughuli za Posta unajumuisha kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za Posta. Katika kuboresha huduma za posta nchini juhudhi mbalimbali zimefanyika na Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Samia Suluhu Hassan pamoja na Wizara na Taasisi zinazoshughulikia masuala ya Anwani za Makazi zimeweza kufuatilia kwa zoezi hilo muhimu ambapo limekuwa na mchango mkubwa sana kwenye Sekta ya Posta na mawasiliano kwa ujumla. Kwa sasa ni rahisi kwa mwananchi wengi kuagiza bidhaa na kuletewa nyumbani au kuuza mtandaoni kwa kuainisha anwani yake ya makazi na postikodi. Matumizi ya anwani za makazi na postikodi yataifanya sekta ya posta kutoa mchango mkubwa zaidi katika kuendeleza uchumi wa kidijiti na uchumi wa buluu kwa vile uuzaji na ununuzi wa bidhaa utafanyika kirahisi, Aidha tayari tunaona mwenendo mzuri wa huduma za utumaji na upokeaji wa vifurushi na vipeto ndani ya nchi kupitia biashara mtandao, au e-commerce. Aidha, TCRA

inaweka viwango vya ubora wa huduma za posta na kupima ufikiwaji wake kwa watoa huduma wote ili kulinda haki za wateja.

2.5 Upangaji na Usimamizi wa Rasilimali za Mawasiliano

Rasilimali za mawasiliano ni pamoja na masafa, namba, vikoa, postikodi na anwani za makazi. TCRA imeendelea kuhakikisha uwepo wa rasilimali zinazowezesha mawasiliano ya simu, Intaneti, redio na televisheni. Usimamizi wa rasilimali hizi umeweza kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Upangaji na usimamizi mzuri wa rasilimali za mawasiliano (masafa na namba), ndio unaowezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano pamoja na huduma za pesa mtandao. TCRA ndio inayopanga na kutoa namba zinazotumika katika mawasiliano pamoja na namba fupi (short codes) zinazotumika katika kufanya miamala ya kifedha na kuwezesha huduma nyingine za ziada. Aidha, TCRA inatoa rasilimali hizi bure kwa wabunifu (Start-ups) mbalimbali wanaotaka kufanya majaribio (testing) kwenye huduma zao kwa kipindi maalum.

TCRA imefanikiwa kugawa masafa yanayowezesha utoaji wa huduma ya intaneti ya kasi. Jitihada hizi zitawezesha wananchi wengi kupata huduma za intaneti ya kasi ambayo ni muhimu sana wakati huu tukiwa kwenye uchumi wa kidijiti. Malengo ya Serikali ni kuhakikisha kuwa, ifikapo mwaka **2025** asilimia **80** ya watanzania wanapata huduma ya intaneti ya kasi. Tunamshukuru Mh. Rais kwa kuendelea kufungua fursa za milango ya TEHAMA ili kufikia lengo hili. TCRA imetoe Masafa yanayowezesha intaneti ya kasi pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kiusimamizi. Aidha, TCRA iko katika hatua za awali za kuongeza ukubwa wa bendi za masafa zilizo huru kutumia (Unlicensed band), hatua itakayoongeza matumizi ya Intaneti kwa kuwa na huduma za intanet za WIFI (hotspots).

2.6 Usimamizi wa usalama mtandaoni

TCRA ina kitengo cha mwitikio wa kukabiliana na majanga ya kompyuta hapa nchini inayojulikana kama ‘Tanzania Central Emergency Response Team’ (TZ-CERT). TZ-CERT ina jukumu la kitaifa la kuratibu mwitikio (Incident Response) wa matukio ya usalama katika mitandao (Cybersecurity) na pia kushirikiana na vyombo vingine vya kikanda na kimataifa katika kusimamia matukio ya usalama wa mtandao. Kitengo hiki huzipatia ufumbuzi changamoto za kiusalama mtandaoni, kufuatilia kwa ukaribu vihatarishi

vya kimtandao na kufanya tathimini za kiusalama ya miundombinu na mifumo muhimu ya TEHAMA kwa lengo la kubaini madhaifu yaliyopo kabla ya mashambulio ya mtandao (cyber-attacks). Kitengo hiki kinaunganisha vitengo vidogo vinavyolinda usalama kwenye sekta za Elimu, Fedha, nk.

2.7 Mifumo ya huduma kwa wateja

TCRA imeendelea kuboresha mifumo ya huduma kwa wateja kama ifuatavyo:

- a) "Tanzanite Portal": Mfumo unaowezesha kuwa na dirisha moja la maombi ya leseni za aina zote, utoaji wa vyeti vya uhakiki wa vifaa vya kielektroniki, kanzi data ya anuani za makazi na dawati la huduma kuwezesha mawasilisho ya malalamiko ya wateja. Mfumo huu ni muunganiko wa moduli zifuatazo:
 - (i.) Moduli inayowezesha TCRA kusimamia na kutoa leseni na nambari za mawasiliano, ukiwezesha watoa huduma kuwasilisha maombi yao bila kufika kwenye ofisi za TCRA;
 - (ii.) Moduli inayowezesha upangaji, ugawaji na ufuutiliaji postikodi za anwani za makazi. Watumiaji (wananchi) wanaweza kupata postikodi za maeneo mbambali kuitia tovuti ya TCRA;
 - (iii.) Moduli inayowezesha TCRA kupokea na kushughulikia maoni, changamoto na taarifa mbalimbali kutoka kwa wateja wake na wanaotaraji kupata huduma za TCRA;
 - (iv.) Moduli inayowezesha utambuzi wa wateja wote wa TCRA, ukibainisha leseni walizonazo, taarifa za kampuni pamoja na taarifa za malipo;
 - (v.) Moduli inayowezesha kusimamia rasilimali za namba (Numbering Management System); na
 - (vi.) Moduli inayowezesha kusimamia uhakiki wa vifaa vya kielektroniki (Online Type Approval).

Mifumo yote inaendelea kuboreshwa ili kuwa rafiki zaidi kwa watumiaji na wananchi wanakaribishwa kuendelea kutoa maoni ili kuboresha zaidi.

- b) TCRA inatoa ushirikiano kwa kuunganisha mifumo yake na taasisi nyingine kama BOT, TRA, NIDA na Gaming Board ili kusaidia kusimamia na kurahisisha upatikanaji wa taarifa.

2.8 Ushiriki wa Tanzania katika shuguhuli za Kimataifa na Kikanda

Tanzania ni mwanachama wa mashirika mbalimbali ya kikanda na kimataifa. TCRA hushirikiana na taasisi za kimataifa na kikanda zinazosimamia mawasiliano na wadhibiti wa mawasiliano katika nchi nyingine na inatekeleza mikataba ya kimataifa katika sekta ya mawasiliano. Baadhi ya Taasisi hizo ni kama zifuatavyo;

(i) Mashirika chini ya Umoja wa Mataifa (United Nation Agencies)

- ✓ Shirika la Mawasiliano Duniani (International Telecommunication Union - ITU);
- ✓ Umoja wa Posta Duniani (Universal Postal Union - UPU);

(ii) Mashirika chini ya Umoja wa Afrika (African Union Agencies)

- ✓ Umoja wa Posta Afrika (Pan African Postal Union - PAPU);
- ✓ Shirika la Mawasiliano Afrika (African Telecommunication Union - ATU);

(iii) Taasisis za Jumuiya ya Madola

- ✓ Conference of Commonwealth Postal Administration (CCPA)
- ✓ Commonwealth Telecommunications Organisation (CTO)

(iv) Taasisi za Kikanda za Mawasiliano: Shirikisho la Wadhibiti wa Mawasiliano Kusini mwa Africa (Communications Regulators' Association of Southern Africa - CRASA), Shirika la Mawasiliano la Africa Mashariki (East African Communications Organization – EACO), Shirikisho la Utangazaji la Kusini mwa Afrika (Southern African Broadcasting Association - SABA) Mtandao wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Afrika (African Communication Regulation Authorities Network – ACRAN).

3.0 MWENENDO WA SEKTA


3.1 Sekta ya Mawasiliano ya Simu na Intaneti

3.1.1 Huduma za Simu

a) Idadi ya Watumiaji wa Simu

Sekta ya Mawasiliano ya Simu nchini imeendelea kukua na hadi kufikia Septemba, 2022 kulikuwa na laini za simu 58.1 Milioni. Idadi hii ya laini za simu inahusisha laini zinatotumiwa na watu na laini zinatumiwa kwa ajili ya mawasiliano kati ya mashine kwa mashine (M2M). Tunao watoa huduma sita (6) kwenye soko letu, yaani Airtel, Vodacom,

Halotel, TTCL, Tigo na Smile. Mgawanyo wa asilimia za soko kwa kila mto huduma ni kama inavyonyesha hapa chini.




Aidha, takwimu zinaonyesha kwamba mikoa mitano (5) Tanzania inayoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya laini za simu zinazotumika yaani (Active SIM-cards) hadi Septemba 2022 ni:- Dar es salaam (Laini Milioni 9,756,697), Mwanza (Laini 3,700,914), Arusha (3,448,200), Mbeya (3,089,848), na Tabora (3,060,407).

b) Gharama za Muunganisho wa simu kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine

Gharama za Muunganisho wa simu kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine zimekua zikipungua mwaka hadi mwaka. Mwaka 2015 gharama zilikua ni TZS 30.58 na kwa sasa (2022) ni TZS 2.00. Hii imesaidia kupunguza gharama za jumla za upigaji wa simu na kuondoa ulazima wa wateja kuwa na simu zaidi ya moja.

Year	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021	2022
Uanishaji Na.3 wa gharama za mwingiliano (Determination No.3 of 2013 (TZS)	30.58	28.7	26.96					
Uainishaji Na.4 wa gharama za mwingiliano (Determination No.4 of 2017				15.60	10.40	5.20	2.60	2.00

c) Mwenendo wa gharama za rejareja kupiga simu bila ya kifurushi Kuanzia 2015 – Sept. 2022 (zikijuisha kodi)




Mwenendo wa gharama za upigaji wa simu nje ya kifurushi zimezidi kushuka kama zinavyoonyeshwa kwenye jedwali hilo juu.

d) Wastani wa Bei za Vifurushi (Tshs)

Wastani wa gharama ya kupiga simu kwa kutumia vifurushi zimekuwa zikibadilika badilika kutokana na gharama wanazotumia watoa huduma kufikisha huduma kwa mteja wa mwisho kubadilika pia. Pamoja na mabadiliko hayo, gharama za kupiga simu ndani na nje ya mtandao zimekuwa na uelekeo wa aina moja wa kupungua na hivyo kumwezesha mteja kuwa na uhuru wa kupiga simu kwenda popote yaani ndani ya mtandao anaoumiliki na nje ya mtandao huo. Hali hii imerahisisha sana mawasiliano na kupunguza ulazima wa kuwa na laini za simu za watoa huduma wote kwa wakati mmoja.

Mwenendo wa gharama za rejareja kupiga simu kwa kutumia kifurushi Kuanzia 2015 – Sept. 2022 (Tax Inclusive)




Vilevile, Mwenendo wa gharama za rejareja kupiga simu kwa kutumia kifurushi kuanzia 2015 mpaka sasa zimekua zikishuka na kuwezesha watu wengi waweze kumudu gharama hizo.

Mwenendo wa gharama ndani na nje ya Mtando zimeendelea kushuka na kukaribiana. Hali hii imechochea shughuli nyingi za kiuchumi kuweza kufanyika kuitia mawasiliano ya simu ukilinganisha na hapo awali. Hivyo kadiri siku zinavyokwenda watoa huduma wamekuwa wakishindana kwa ubora wa huduma wanayoitoa na sio gharama walizonazo kwa wateja wao. Hali hii ya kushindanisha huduma utamwezesha mteja kupata huduma bora zaidi kwani gharama kwa watoa huduma wengi zinafanana.

e) Gharama za SMS

Mwenendo wa bei za rejareja kwa SMS bila kifurushi na kwenye Kifurushi Kuanzia 2015 – Septemba 2022 (Tshs – zikhushisha kodi) nazo zimeendelea kushuka kwa sababu ya ushindani katika sekta.



f) Uwiano wa Mawasiliano ya simu kwa Idadi ya watu

	2022
IDADI YA WATU	61.7 Milioni
Uwiano wa Mawasiliano ya simu ya 2G kwa Idadi ya watu (2G Population Coverage)	96%
Uwiano wa Mawasiliano ya simu ya 3G kwa Idadi ya watu (3G Population Coverage)	72%
Uwiano wa Mawasiliano ya simu ya 4G kwa Idadi ya watu (4G Population Coverage)	55%
Uwiano wa Mawasiliano ya simu kwa maeneo ya kijiografia (Geographical Coverage)	66%
Asilimia ya Simu Janja (Smartphone Penetration)	25%


Uwiano baina ya mitandao na matumizi yanaonyesha kuwa maeneo mengi yamefikiwa na huduma za Intanet ila watumiaji ni wachache hivyo kuna haja ya kuongeza upatikanaji wa simu janja. Pia mwelekeo wa kufikia lengo la serikali la asilimia 80% ya watumiaji wa huduma za Intanet zinaendela vema.

3.1.2 Huduma za Intaneti

Takwimu za sasa zinaonesha matumizi ya Intaneti yameongezeka kwa asilimia 4.2 kutoka milioni **29,858,759**, mwaka 2021 hadi kufikia **31,122,163** mwezi Septemba 2022. Idadi ya watumiaji wa intaneti kwa sasa wamefikia 31,122,163. Mwelekeo wa ongezeko la watumiaji wa intaneti linaonesha kwamba kulikuwa na ukuaji wa takriban asilimia 17 kila mwaka, katika kipindi cha miaka 5 ambapo mwaka 2017, kulikuwa na watumiaji Milioni 16,106,636 na mwishoni mwa mwaka 2021 waliongezeka kufikia **Milioni 29,103,482**. Ongezeko la matumizi ya intaneti limechangiwa pia na matumizi ya Kiswahili. Maudhui ya Kiswahili kwenye intaneti yanaongezeka kwa kasi na Program tumizi (applications) kwa lugha ya Kiswahili zimeongezeka pia. Kumekuwa na juhudzi za kuendeleza na kueneza matumizi ya Kiswahili kimataifa.


a) Wastani wa Bei za Data (Tshs)

Mwenendo wa gharama za rejareja za data bila kifurushi na kwenye kifurushi Kuanzia 2015 – Sept 2022 (Tax Inclusive) zimeendele kushuka na kuongeza utumiaji wa huduma za Intanet nchini.




b) Idadi ya Watumiaji wa Mitandao ya Kijamii

Takwimu za ripoti hii ya utendaji wa sekta ya Mawasiliano nchini zinabainisha mitandao mitano (5) ya kijamii inayotumiwa zaidi, hivyo kuongoza kwa kiwango kikubwa cha data iliyotumika kwa kipimo cha GB; ambapo Mtandao wa kijamii wa FaceBook uliongoza kwa kurekodi (GB Bilioni 2.59), ukifuatiwa na YouTube wenyewe (GB Bilioni 1.91), kisha WhatsApp uliokuwa na (Bilioni 1.58), na TikTok ukiwa na (GB Milioni 999) ikifuatiwa na mitandao mingine.



3.1.4 Huduma za Kifedha katika Mtandao wa simu

Tanzania inazidi kuendeleza mfumo jumuishi wa kifedha kutoptana na kuongezeka kwa watumiaji wanaofanya miamala kupitia simu za mkononi. Takwimu za mawasiliano za mwezi Septemba 2022 zinaonyesha kwamba huduma za pesa kupitia simu za mkononi zimeongezeka. Akaunti za pesa kwa simu za mkononi zimeongezeka na kufikia **39,590,502**.



Idadi ya miamala imeongezeka kutoka Bil. 349,952,830 hadi miamala Bil. 366,178,409 Septemba 2022.

Aidha, akaunti za pesa kwa simu zimeongezeka kwa asilimia 1.5 katika miezi tisa iliyopita; kuanzia Januari hadi Septemba 2022; wakati miamala ikiongezeka kwa asilimia 2.

Mwezi	Mwaka	Idadi ya Watumiaji	Idadi ya Miamala	Thamani ya Miamala (TZS)
JANUARI	2022	35,201,960	308,569,751	10,350,248,535,456
FEBRUARI	2022	35,578,052	292,626,474	9,539,172,477,200
MACHI	2022	35,749,298	330,148,997	10,703,041,422,029
APRILI	2022	36,068,839	327,324,035	10,321,267,168,688
MEI	2022	36,302,884	352,362,035	10,689,193,723,704
JUNI	2022	37,407,233	343,639,879	11,608,009,683,538
JULAI	2022	38,008,482	349,952,830	12,548,569,958,747
AGOSTI	2022	38,504,971	356,790,863	12,741,158,372,863
SEPTEMBA	2022	39,590,502	366,178,409	12,722,059,888,707

3.2 Sekta ya Utangazaji

Takwimu za utangazaji zinaonyesha kwamba visimbuzi 3,326,845 vilikuwa hewani hadi Septemba 2022. Kati ya hivyo, 1,656,460 ni vya dijitali kwa mfumo wa televisheni wa utangazaji wa mitambo ya ardhini (DTT) kulinganisha na 1,670,385 kwa mfumo wa televisheni kwa satelaiti.

Dar es Salaam inaongoza kwa kuwa na visimbuzi (1,270,755), ikifuatiwa na Arusha (272,702), Mwanza (261,237) na Mbeya (218,007). Mikoa yenyе visimbuzi vichache ni Songwe (1,568) ukifuatiwa na Katavi (16,990).

Televisheni za waya (cable tv) zimeenea kutoka watu 16,786 waliouunganishwa 2018 hadi 41,092 Septemba 2022. Huduma ya televisheni kwa waya (yaani cable Tv) imeenea mikoa ya Ziwa; ambapo mkoa wa Simiyu unaongoza; ukiwa na jumla ya waliouunganishwa 4,584, ikifuatiwa na Mwanza, yenyе 3,480.

Idadi ya Dikoda zinazotumika kwa kila Mto Huduma kufikia Septemba, 2022

MTOA HUDUMA	DTT	DTH	JUMLA
Agape	2,023	1,978	4,001
Azam	100,389	787,570	887,959
Continetal	40,411	26,540	66,951
DiGiTek	17,392	0	17,392
DSTv	0	230,943	230,943
Star Times	1,496,245	591,914	2,088,159
Zuku	0	31,440	31,440
JUMLA	1,656,460	1,670,385	3,326,845

3.3 Huduma za Posta

Huduma za utumaji na upokeaji wa vifurushi na vipeto ndani ya nchi zinazidi kushamiri na kuchochaea ukuaji wa biashara mtandao ambapo kwa robo mwaka ya kwanza ya 2022 vifurushi viliviyotumwa ni 513,080. Katika Sekta hii ya Posta pia tumetuma kwenda nje ya nchi jumla ya vifurushi na vipeto 49,286 na kupokea 21,962 huduma hii inaendelea kuchagiza ukuaji wa biashara mtandao au e-commerce.


Mwenendo wa Vifurushi na Vipeto vilivyotumwa na kupokelewa nchini

Year	2017	2018	2019	2020	2021
Posted to Int	10,121,388	5,098,728	2,873,312	1,116,069	564,528
Delivered from Int	2,339,149	7,999,942	3,927,692	1,391,829	958,121



Aidha, siku za karibuni tumeshuhudia kupungua kwa watoa wa huduma za posta kutokana na changamoto zinazotokana na maendeleo ya TEHAMA ambayo yameleta njia mbadala wa mawasiliano na kuzuka kwa janga la homa kali ya mapafu inayoletwa na virusi vya UVIKO 19 kumeathiri posta. Kampuni binafsi za huduma za posta na usafirishaji vifurushi (courier companies) zimepungua kutoka 128 mwaka 2021 hadi 90 mwaka 2022.

3.4 Upatikanaji wa huduma za Mawasiliano kwenye maeneo yenye changamoto

Katika jitihada za kuhakikisha wanachi wote wanapata huduma bora za mawasiliano, TCRA kwa kushirikiana na UCSAF, TAMISEMI na wadau wengine imeendelea kufanya Ukaguzi na kuanisha maeneo ambayo upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu bado zina changamoto. Kwa mfano katika maeneo ya Visiwa vinavyozunguka Unguja na Pemba kama inavyoonekana hapa chini: Moja ya matunda ya juhudhi hizi ni pamoja na uzinduzi wa Minara 45 ya Mawasiliano uliofanyika Zanzibar hivi karibuni.



Na mfano mwagine ni katika maeneo pembezoni mwa Ziwa Viktoria na Ziwa Tanganyika kama inavyoonekana hapa chini:-



3.5 Usalama kwenye Mitandao (Cyberspace)

TCRA imeendele kusimamia anga la mtandao na kuhakikisha liko salama na TCRA itaendelea kushauri juu ya hatua za kurekebisha na kulinda mifumo na miundombinu ya

mtandao dhidi ya mashambulio mtandaoni. Katika kushughulikia masuala ya Usalama mtandaoni TCRA ilialikwa na Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) kushiriki kwenye Global Cybersecurity Index (GCI) v4, GCI inapima jitihada za nchi wanachama katika masuala ya usalama wa mtandao (cybersecurity). Matokeo ya GCI yaliyotolewa Juni, 2021, yalionyesha kuwa Tanzania inashika nafasi ya pili (2) barani Afrika na nafasi ya thelathini na saba (37) kimataifa.

4.0 CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA MAWASILIANO NA UTATUZI WAKE

TCRA katika kutekeleza majukumu yake ilikabiliana na changamoto na utatuzi wake umeainishwa kama ifuatavyo:

Na	Aina ya Changamoto	Namna ya kukabiliana na changamoto
1.	Uharibifu wa Miundombinu ya Mawasiliano	TCRA imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kwenye kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuilinda miundombinu ya Mawasiliano.
2.	Utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa bado.	TCRA imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kama UCSAF, Watoa huduma za mawasiliano, TANESCO, Wakala wa Umeme Vijijini (REA), Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) pamoja na kuchangia katika Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ili kuhakikisha kuwa huduma za Mawasiliano zinafikishwa kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa. Aidha, TCRA imeendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa watoa huduma wanaendelea kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma wanazotoa kama inavyoelekezwa kwenye masharti ya lesseni walizopewa ikiwa ni pamoja na kuchangia katika mfuko wa Mawasiliano kwa wote.
3.	Mahitaji makubwa ya bendi za masafa	TCRA inaendelea kusimamia upangaji,

Na	Aina ya Changamoto	Namna ya kukabiliana na changamoto
	ukilinganisha na masafa yaliyopo.	ugawaji na matumizi bora ya masafa ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba rasilimali hizi adimu zinatumika ipasavyo kwa maslahi mapana ya Taifa katika kujenga uchumi wa kidijiti.
4.	Usalama wa Mtandaoni na Uhalifu wa Mtandaoni (Cyber security and Cybercrime).	TCRA kupitia kituo cha Kitaifa cha Usalama Mtandaoni (TZ-CERT) imeendelea kukabiliana na uhalifu mtandaoni ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wadau.
5.	Kudhibiti Maudhui ya mtandaoni	TCRA inaendelea kuboresha na kusimamia ipasavyo kanuni za Mawasiliano ya kielectroniki na postal (online contents) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile Jeshi la Polisi, BASATA, Mahakama n.k.
6.	Ubora wa Huduma za Mawasiliano	TCRA imeendelea kusimamia ubora wa huduma za mawasiliano kwa kutumia mitambo ya kisasa ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na watoa huduma zinakidhi viwango bora.

5.0 MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZILIZOPANGWA KWA MWAKA 2022/23

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

- i) Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi ikiwa ni pamoja na mafunzo endelevu ili kukuza uwezo katika utekelezaji wa kazi za kusimamia sekta ya Mawasiliano;
- ii) Kupanga na kufatilia rasilimali za mawasiliano (masafa, namba, vikoa na postikodi) pamoja na miundombinu ya Mawasiliano kwa mujibu wa sheria, kanuni na kwa kuzingatia masharti ya leseni;

- iii) Kupima na kusimamia ubora wa huduma za mawasiliano ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za Mawasiliano zinazokidhi viwango vya kimataifa;
- iv) Kudhibiti mawasiliano ya simu za ulaghai katika mitandao ya makampuni ya simu ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali na watoa huduma za Mawasiliano ya simu;
- v) Kutoa leseni pamoja na kuimarisha usimamizi wa mfumo wa utoaji leseni na rasilimali za mawasiliano;
- vi) Kutoa elimu kwa watumiaji na wadau wengine wa huduma za mawasiliano ili kuongeza uelewa juu ya haki na wajibu wao;
- vii) Kuimarisha ushirikiano na wadau wa mawasiliano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kuhakikisha usimamizi shirikishi wa sekta;
- viii) Kuendelea kuimarisha Mifumo ya huduma kwa wateja ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na wadau wa sekta ya mawasiliano; na
- ix) Kuendelea kuhakikisha usalama wa mitandao ya kompyuta ili kupunguza mashambulizi ya kmtandao;
- x) Kuendelea kuwashirikisha watoa huduma za mawasiliano katika maamuzi mbalimbali yanayohusu Sekta ya Mawasiliano ili kuweza kukuza Sekta na kufikia uchumi wa Kidijiti.

6.0 HITIMISHO

TCRA inaendelea kusimamia Sekta ya Mawasiliano ikiwa ni pamoja na kushirikiana na wadau mbalimbali katika ngazi ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kuhakikisha Sekta ya Mawasiliano inatoa mchango katika maendeleo ya nchi na kuwa kichocheo cha ukuaji wa uchumi wa kidijiti na uchumi wa buluu.

**IMETOLEWA NA
MKURUGENZI MKUU
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
03 NOVEMBA 2022**